# KIGEZO CHA DINI

**Na**

**Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian**

Masihi Mau'udi na Imam Mahdi
Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya
Tanzania

# Kigezo Cha Dini

Mi'yārul-Madhāhib (Kiurdu)

Mwandishi:
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi

Mfasiri: Sheikh Yusufu Athumani Kambaulaya

© Islam International Publications Ltd.

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): Qadian 1895
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): Tanzania 2016

Kwa maelezo zaidi:
Tanzania:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dare es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744
Kenya:
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi, Kenya. Simu: +255222111031

Kimechapwa na: Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salam, Tanzania
Simu: +255222111031

ISBN: 185372863-2

رسالہ

# معیار المذاہب

## فطرتی معیار سے مذاہب کا مقابلہ

از تصنیف

حضرت مسیح موعود علیہ السلام

Tafsiri ya jalada la chapa ya kawanza

Kijitabu

# KIGEZO CHA DINI

Malinganisho ya dini kwa kigezo
cha asili

Na

Hadhrat Masihi Mau'udi[as]

# MAELEZO YA MWENEZI

Alhamdulillahi, kitabu kingine tena cha Seyidna Ahamad a.s., Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kimepata kufasiriwa kwa Kiswahili. Kitabu chenyewe kipo kwa Kiurdu kinachoitwa Mi'yarul-Madhahib, yaani Kigezo Cha Dini.

Kitabu hiki kinalinganisha mafundisho kumhusu Mwenyezi Mungu yaliyofundishwa na dini tatu, Uaria, Ukristo na Uislamu, na kubaninisha kinagaubaga fundisho lipi miongoni mwa mafundisho hayo lawiana na kigezo asilia cha kupimia ukweli wa dini.

Aliyekifasiri ndiye Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya. Kisha Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, Amiri na Mbashiri Mkuu wa zamani wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Tanzania na Sheikh Adnan Ahmad Hashimi, mbashiri wetu nchini Kenya, waliidurusu na kurekebisha huko na huko. Mwishowe kabla ya kuipeleka mtamboni, nikailinganisha kwa uangalifu na matini ya Kiurdu, na kuboresha sehemu mbalimbali. Isitoshe, sheikh

Ansar Hussain na Seyid Tanwir Mujtaba walisaidia katika kazi hii kwa njia mblaimbali.

Hili ni zao la Dawati la Kiswahili.

Jamil R. Rafiq
Wakilut Tasnif, Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan.

14 Aprili 2016

# Kijitabu “Kigezo cha Dini”

## Malinganisho ya dini kwa kigezo cha asili na maelezo kidogo ya hisani ya Serikali ya Kiingereza

Nionavyo, hakuna fursa nzuri zaidi inayoweza kupatikana kwa wananchi wa nchi yoyote ya kuzichunguza na kuzikagua na kupambanua dini halisi na zisizo halisi kama ilivyopatikana kwa nchi yetu ya Panjab na India. Kwa kupata nafasi hii, fadhili ya kwanza ya Mwenyezi Mungu ni Serikali ya Kiingereza kuitawala hii nchi yetu. Sisi tutakuwa watovu wa shukrani sana na wenye kuikana neema kama hatutaishukuru kwa moyo wa kweli Serikali hii mhisani ambayo kwa baraka za kuwepo kwake sisi tumepata nafasi ya kuwaita watu na kuwahubiria Islam, ambayo nafasi hiyo kabla yetu hata mfalme yeyote hakuweza kuipata. Maana, serikali hii ipendayo elimu imetoa uhuru wa kueleza maoni, ambao mfano wake ukitaka kutafuta ndani ya utawala wowote wa siku hizi ni kazi bure. Je, si jambo la ajabu kwamba masokoni mwa London tunaweza kutoa mawaidha kuthibitisha dini ya Kiislamu, ambayo haiyumkiniki tupate nafasi hiyo hasa katika mji

Mtakatifu wa Makka. Na Serikali hii si tu iliitolea kila kaumu uhuru wa kuchapisha vitabu na kueneza dini, bali ikalisaidia kila kundi kwa kueneza elimu na ufundi wa aina mbalimbali na imefumbua macho ya dunia kwa elimu na malezi. Ingawa hisani hii ya Serikali hii mhisani siyo ndogo kwamba inazilinda kwa moyo wa ukweli mali, heshima na damu zetu kadri iwezekanavyo na inatunufaisha kwa uhuru huu ambao kwa kuutafuta wengi wenye huruma ya kweli ya wanadamu wamekufa kabla yetu, lakini hisani ya pili ya Serikali hii inaizidi hiyo kwamba inakusudia kuwafanya washenzi wa porini na wanadamu wa jina tu wawe watu wenye elimu na akili kwa kuwatolea elimu ya aina aina. Twaona kuwa kwa juhudi zinazofululiza za Serikali hii watu waliokuwa kama mifugo na wanyama wameshapata sehemu ya utu, ujuzi na busara kiasi fulani. Na katika mioyo na akili ya watu wengi mmezalika mwanga unaozalika baada ya kuelimika, kana kwamba upanuzi wa elimu umeibadilisha dunia mara moja. Lakini jinsi ambavyo kwa kupenya kioo mwanga unaweza kuingia ndani ya nyumba lakini maji hayawezi kuingia, ndivyo ambavyo mwanga wa kielimu umeishaingia ndani ya nyoyo na bongo zao lakini bado maji safi ya ikhlasi na ya kuelekea kwenye haki hayajaingia ndani ambayo kwayo mmea wa kiroho ungestawi na ungezaa matunda mazuri. Lakini hili si kosa la serikali, bali

hivi sasa sababu zenyewe hazipo au zipo chache sana zisisimuazo hali ya kiroho ya ukweli. Ni jambo la ajabu kuwa kutokana na maendeleo ya kielimu, hata udanganyifu na ujanja nao unaonekana kuzidi kiasi fulani, na watu wa haki wanakabiliana na wasiwasi mwingi usiovumilika. Unyofu wa imani umepungua sana, na mawazo ya kifalsafa yasiyofuatana na ujuzi wa dini yamewatilia wasomi wapya athari yenye sumu inayowavutia kwenye kumkana Mungu. Na kwa kweli ni vigumu sana watu waweze kuepukana na athari hiyo pasipo kukingwa na mafundisho ya kidini. Basi, ole wake aliyeachwa ndani ya madrasa na vyuo ilhali hana habari ya maarifa ya dini na kweli zake. Naam tunaweza kusema kuwa serikali hii yenye uthabiti mkubwa inayowahurumia wanadamu, ikaisafisha ardhi ya nyoyo za nchi hii kame kwa kufyeka, kwa juhudu kubwa, miti ya porini na magugu na nyasi za aina aina zilizokuwa zimeifunika ardhi kwa sababu ya kuwa ndefu sana. Na sasa kwa kiasili wakati umewadia kwamba mbegu za ukweli zipandwe katika ardhi hii na kisha zinyweshelezwe kwa maji ya kimbingu. Basi, ni wenye bahati njema sana wale watu ambao kwa kupitia serikali hii yenye baraka wamezikaribia mvua za kimbingu. Waislamu wanapaswa waielewe serikali hii kuwa fadhili ya Mwenyezi Mungu na wajitahidi kuitii kikwelikweli ili wawe mfano kwa wengine. Je malipo ya hisani siyo

hisani? Je wema haulazimiki kulipwa na wema? Hivyo, inatakiwa kila mtu afikirie na aonyeshe ustadi wake mwema. Sheria ya Kiislamu haitaki kupoteza ihsani au haki ya yeyote yule. Basi, si kwa unafiki bali kwa moyo wa kweli yapasa kuitii serikali hii mhisani, maana kwa kueneza mwanga wa dini yetu Mwenyezi Mungu Ameiweka hii kuwa njia ya kwanza.

Kisha njia ya pili iliyozuka nchini mwetu ya kutambua dini ni wingi wa viwanda vya uchapishaji, maana, vitabu vingi ambavyo kana kwamba vilikuwa vimefukilika, vimefufuka kwa njia ya viwanda vya uchapishaji hata kwamba Veda ya Mabaniani nayo imejitokeza ikivaa vazi la karatasi kama kwamba imezalika upya, na hivyo imefichua visa vilivyotungwa na wajinga na watu wa kawaida.

Njia ya tatu ni ya kufunguliwa kwa njia na utaratibu mzuri wa posta na vitabu kuwasili nchini humu kutoka nchi za mbali na kutoka hapa kuvienda nchi hizo. Njia hizo zote ni za kuuchunguza ukweli ambazo fadhili ya Mwenyezi Mungu imeziweka nchini mwetu, ambazo tunafaidika nazo kwa uhuru kamili. Faida zote hizo tumezipata kwa njia ya serikali hii mhisani na yenye nia njema, ambayo kwa ajili yake dua zinatoka zenyewe moyoni mwetu. Lakini swali likizuka kwamba kwa nini basi serikali iliyostaarabika na yenye busara inafungamana na dini ambamo kwa

kumfanya mwanadamu kuwa mungu, Mungu wa kweli Anavunjiliwa jalali yake ya dhahiri ya azali na isiyobadilika, basi ni masikitiko makubwa kuwa hakuna jibu la swali hili isipokuwa tu kwamba fikara za masultani na wafalme za kutawala zinapopita mipaka ya kawaida, basi nguvu zote za kutaamali na kutafakari huishia mumo humo na maslahi ya himaya ya utaifa hayawaachii fursa kuangalia mambo ya Akhera, na vivyo hivyo kwa kubanwa na matakwa ya kidunia yanayofululiza yasiyokoma, jazba ya kumtambua Mungu na kutafuta ukweli hupungua. Hata hivyo, kwa fadhili za Mwenyezi Mungu sikati tamaa kuwa Yeye Aielekeze serikali hii hodari kwenye njia iliyonyooka. Kama tunavyoiombea serikali hii wema wa kidunia, vivyo hivyo tuiombeavyo kwa ajili ya akhera yake pia. Basi kuna ajabu gani kwetu sisi kuziona athari za dua.

Katika zama hizi ambapo njia nyingi za kupambanua ukweli na batili zimepatikana, nchini mwetu kuna dini tatu zinazokabiliana na kugongana zenyewe kwa zenyewe. Katika dini zote hizo tatu kila mfuasi wa dini anadai kuwa dini yangu tu ndiyo ya kweli na ndiyo sahihi. Ajabu ni kwamba hakuna mtu anayeelekea kukiri kuwa dini yake haiko kwenye misingi ya ukweli. Lakini mimi siwezi kukubali jambo hili kuwa kama yalivyo madai ya wapinzani wetu,

vivyo hivyo mioyo yao nayo yaweza kuafikiana na ndimi zao hata kwa sekunde moja. Alama moja kubwa ya dini ya kweli ni hii kuwa kabla hatujaeleza dalili za ukweli wake, dini hiyo yenyewe huwa inang'aa na kuangaza kiasi kwamba kama dini zingine zikilinganishwa nayo, hizo zote zitaonekana ziko gizani. Na mtu mwenye busara anaweza kuielewa hoja hiyo barabara aangaliapo mafundisho ya asili ya kila dini kwa kuitenganisha na hoja zake za kuzushwa. Yaani azipime njia za dini hizo za kumtambua Mungu kwa kulinganisha kila moja na nyinginezo, na asiiongezee itikadi ya kumtambua Mungu ya dini yoyote hoja za nje. Bali kwa kuondolea mbali hoja zote, aichunguze dini moja kwa kuilinganisha na dini nyingine na afikirie kuwa ndani ya dini ipi umo mng'ao wa ukweli wa dhati, na dini gani ina sifa hii kwamba kuiangalia tu njia yake ya utambuzi wa Mungu huivutia mioyo kwake. Mathalani, dini zile tatu nilizozitaja sasa hivi ni hizi: 1. Uaria, 2. Ukristo, 3. Uislamu. Tukitaka kuonyesha sura halisi ya dini hizo tatu, basi maelezo ndiyo yafuatayo:

Dini ya Uaria ina mungu ambaye uungu wake hauwezi kujiendesha kwa nguvu na uwezo wake wa dhati, na matumaini yake yote yanavitegemea vitu ambavyo havikuumbwa kwa mikono yake. Siyo kazi ya mwanadamu kujua upeo wa kudura za Mungu wa kweli, lakini nguvu za Parmeshar wa Waariya

zinaweza kuheshabiwa kwa vidole. Parmeshar huyo ana mtaji haba kiasi kwamba mpaka wa nguvu zake umeisha julikana. Na kama kudura zake zikisifiwa sana sana, basi hatuwezi kusema zaidi ya hii kwamba yu fundi wa kuviunganisha vitu vilivyopo tangu azali kama yeye, kama wafanyavyo waashi. Na kama ikiulizwa anaongeza kitu gani kutoa kwake mwenyewe, kwa masikitiko makubwa twalazimika kusema kwamba hamna chochote! Ilmuradi, upeo wa mwisho wa nguvu zake ndio tu kuwa anaziunganisha roho na miili midogo midogo ambavyo ni vya kale na vipo tangu azali kama alivyokuwepo yeye mwenyewe, na uwepo wake haukuathiri kazalika kwao. Lakini kujenga hoja juu ya jambo hili ni vigumu kwamba kwa nini vitu hivyo vilivyo tangu azali vinamhitaji Parmeshar kama huyo ilhali vitu vyote vipo vyenyewe tu, nguvu zao zote pia zipo zenyewe tu, na zina uwezo pia wa kuungana zenyewe kwa zenyewe, ndani yao mna nguvu za kuvutana pia tangu azali, na sifa zao zote zidhihirikazo baada ya kuchanganyikana pia zipo tu zenyewe, hapo haieleweki kuwa kwa dalili gani inathibitika haja ya kuwepo kwa Parmeshar huyo mpungufu, asiye na nguvu. Na yaweza kuwa tofauti gani basi baina yake na ghairi yake isipokuwa ujanja na akili! Kuna shaka gani ndani yake kuwa Parmeshar wa Waaria ameshindwa kuwa na zile nguvu zisizo na kikomo zihusikanazo na ukamilifu wa Uungu. Na hii

ni bahati mbaya ya Parmeshar huyu wa kubuniwa kuwa haukuweza kupatikana kwake ukamilifu utimilifu unaolazimu kwa mng'ao kamili wa jalali ya Uungu. Na bahati mbaya ya pili ni hii kuwa kuacha kurasa chache za Veda hakuna njia yoyote ya kumtambua kwa mujibu wa kanuni ya asili. Maana, kama ni kweli kuwa roho na chembechembe za miili, pamoja na nguvu zao na mivutano yao na sifa zao na akili zao na fahamu zao na ujuzi wao, vipo vyenyewe tu, hapo akili timamu haioni haja ya mtu mwingine kwa kuviunganisha hivyo vitu. Kwani katika hali hii haiwezekani kujibu swali hili kuwa vile vitu vilivyopo tangu azali, vyenyewe ni miungu ya uwepo wao navyo vina nguvu zote ndani mwao zilizolazimu kwa kuviunganisha pamoja, basi, ikiwa havikumhitaji Parmeshar kwa ajili ya uwepo wao, wala havikumhitaji mtengenezaji yeyote wa nguvu zao na sifa zao, sasa kwa sababu gani kwa kuungana pamoja vimemhitaji mwingine aviunganishaye ilhali kuziunganisha pamoja roho na nguvu zao, na kuziunganisha pamoja chembechembe za miili na nguvu zao pia ni aina moja ya muunganisho. Basi kwa hiyo imeshathibitika kuwa jinsi ambavyo vitu vilivyo tangu azali havihitaji muumbaji kwa ajili ya kuwepo kwao wala havihitaji mvumbuzi kwa ajili ya nguvu zao pia, ndivyo ambavyo hakuna haja ya fundi yeyote kwa ajili ya kuviunganisha pamoja. Huu utakuwa ni ujinga

mkubwa kwamba kwanza kwa ndimi zao wenyewe wakubali kuhusiana na hivyo vitu kuwa havimhitaji mwingine kwa ajili ya kuwepo kwao na nguvu zao na mafungamano yao, kisha kwa kinywa hicho hicho waseme kuwa lazima kuna haja ya mwingine kwa kuviunganisha baadhi ya vitu. Basi hili litakuwa ni dai lisilokuwa na hoja. Ilmuradi, kutokana na itikadi hii itakuwa vigumu kuthibitisha hata kuwepo kwa Parmeshar. Basi hakuna mtu mwenye bahati mbaya zaidi kuliko yule anayemtegemea Parmeshar ambaye hakuweza kupata sababu nzuri za kuthibitisha hata kuwepo kwake kwa sababu ya kupungukiwa uwezo. Hizo ndizo nguvu za kiungu zilizomo ndani ya Parmeshar wa Mabaniani. Na hali ya nguvu za kikhulka ndiyo kwamba zinaonekana ni nyonge zaidi kuliko hata nguvu za wanadamu. Maana, tunaona kuwa mtu mwema mara nyingi huwasamehe makosa ya wakosaji wanaomuomba msamaha kwa adabu na unyenyekevu, na mara nyingi kwa sifa ya ukarimu wa nafsi yake huwafanyia watu hisani ambao wanakuwa hawana haki yoyote. Lakini Waariya wanaeleza kumhusu Parmeshar wao kuwa yeye hana bahati ya kuwa na khulka za aina zote hizo mbili, na kwao kila kosa husababisha roho kuzaliwa kwa sura mbalimbali mara mamilioni kwa mamilioni, na mfanya dhambi hapati kuachiliwa pasipo kuadhibiwa kikamilifu kwa kuzaliwa kwa sura tofauti nyingi zisizohesabika. Na

sawa na itikadi yao, ni bure kutumai kwamba toba ya mtu, majuto na kuomba ghofira vitamkinga asipate kuzaliwa mara nyingine kwa sura tofauti, au kuelekea kwake kwenye haki kutamlinda kupata adhabu ya kauli zake na amali zake zisizo haki. Bali hakuna budi kupitia kuzaliwa mara nyingi zisizohesabika kwa sura tofauti — jambo ambalo haliwezi kuepukika. Na kusamehe kwa ukarimu na hisani siyo mazoea ya Parmeshar. Hali njema aliyo nayo mtu au mnyama au neema yoyote aipatayo ni tunda la kipindi kimojawapo alichoishi zamani. Lakini ni masikitiko kuwa ingawa Waariya wanajivunia sana mafundisho ya Veda, lakini hata hivyo fundisho hili batili la Veda halikuweza kuishinda dhamira yao ya kibinadamu. Nami nameona mara kwa mara kwa sababu ya kukutana mara nyingi na baadhi ya wafuasi wa dhehebu hilo kwamba jinsi wakati wa kuongelea *Neyoga*, Waaria wanavyoaibika, vivyo hivyo wao wapatavyo aibu sana waulizwapo kwa nini nguvu za kiasili na za kikhulka za Parmeshar zimekadirika kiasi kwamba kutokana na shida hiyo hata uungu wake hauwezi kuthibitika kiakili na kwa sababu hiyo Waaria wenye bahati mbaya walikosa kupata wokovu wa milele. Ilmuradi, hakika na asili ya Parmeshar wa Mabaniani ndiyo hii tu kwamba yu mnyonge sana katika nguvu za kikhulka na kiungu na anastahiki kuhurumiwa. Na labda hii ndiyo sababu kuwa ndani

ya Veda kwa kuacha ibada ya Parmeshar, ibada ya moto, upepo, mwezi, jua na maji imetiliwa mkazo, na kila upaji na zawadi vimeombwa kwa vitu hivyo. Kwani Parmeshar asipoweza kuwafikisha Waariya kwenye makusudio yoyote, bali yeye mwenyewe anaishi katika hali ya kutokufanikiwa kwa kukosa kudura zilizo kamilifu, basi mtu kumtegemea yeye ni kosa kabisa. Kwa kuonyesha picha kamili ya Parmeshar wa Mabaniani, yanatosha tuliyoishaandika.

Sasa dini ya pili, yaani Ukristo, imebaki ambayo wafuasi wake wanamfikiria mungu wao — wanayemwita Yesu Masihi kwa nguvu na harara na kwa kupiga chuku — kuwa mungu wa kweli. Na sura ya mungu wa Wakristo ni hii kuwa yeye ni mwana wa Mwisraeli mmoja, Mariamu binti Yakubu, ambaye baada ya kufikia umri wa miaka 32 akaiaga dunia. Tunapofikiria wakati wa kukamatwa namna alivyoshindwa kupata muradi wake baada ya kufanya maombi usiku kucha, akakamatwa kwa dhila, na sawa na kauli ya Wakristo akatundikwa msalabani na akafa akilia “Eloi Eloi”, mara mwili wetu unatetemeka kuwa je mtu ambaye dua yake haikukubaliwa na Mungu na akashindwa kupata muradi wake, akafa akiendelea kupigwa, je tunaweza kumwita Mungu Mweza. Hebu iwekeni mandhari ya tukio hilo mbele ya macho yenu

pale Yesu Masihi akiwa mahabusu alipopelekwa kwa Herode kutoka mahakama ya Pilato. Hii ndiyo shani ya kiungu kuwa akiwa mahabusu ametiwa pingu mikononi, minyororo miguuni akipelekwa mahakama chini ya ulinzi wa maaskari wachache na kukemewa, akaondoka kuelekea Galilaya. Na katika hali hii ya kuwa na moyo mzito akafikia mahakama baada ya mahakama. Pilato akataka kumwachia huru kama akiona mwujiza, lakini hakuweza kuonyesha mwujiza wowote. Yote yaliposhindikana akarejeshwa tena korokoroni na akakabidhiwa kwa Wayahudi, na mara moja wakammaliza uahi wake.

Sasa wasomaji wenyewe wafikirie kwamba je hizo ndizo alama za Mungu wa kweli na wa hakika? Je, dhamira safi inaweza kulikubali jambo hili kuwa yule Aliye Muumbaji wa mbingu na ardhi na Mmiliki wa kudura na nguvu zisizo na kikomo, mwishoni ageuke kuwa mwenye bahati mbaya, mnyonge na dhalili kiasi hiki kwamba watu wakorofi wamsagilie mbali katika mikono yao. Kama mtu akimwabudu mungu kama huyo na kumtegemea yeye, basi anayo hiari. Lakini, ukweli wenyewe ni kuwa kama mungu wa Wakristo akilinganishwa na Parmeshar wa Waariya na kupimwa nguvu na kudura zake, yeye ataonekana mbele yake kuwa si chochote. Kwani, Parmeshar wa kubuniwa wa Waaria ingawa hanao uwezo wa

kuumba kitu, lakini wanaseme anaweza kuviunganisha kiasi fulani vitu vilivyokwisha umbika. Lakini ndani ya Yesu wa Wakristo hata uwezo kiasi hicho pia haukuthibitika. Pale Wayahudi walipomtundika msalabani na wakasema kuwa sasa kama ukijiokoa, tutakuamini, yeye hakuweza kujiokoa mbele yao, ilhali haikuwa kazi kubwa kujiokoa, ilikuwa tu kuunganisha mwili wake na roho yake pamoja. Lakini huyu mdhaifu hata hakupata uwezo wa kuunganisha. Baadaye wasiri wakazua maneno kuwa yeye akafufuka kaburini. Lakini inasikitisha kwamba hao hawakufikiria kuwa walilotaka Mayahudi lilikuwa ni kuwa afufuke mbele yetu. Na kwa vile hakufufuka mbele yao wala baada ya kufufuka kaburini hakuja kukutana nao, basi kwa Mayahudi bali kwa kila mtafiti kuna uhakikisho gani ya kuwa kweli kafufuka? Na pasipo uhakikisho hata kama idhaniwe kuwa maiti ilipotea kaburini, ufufuko hauwezi kuthibitika, bali kiakili inathibitika kwa yakini hii tu kuwa mwenye kuonyesha "mwujiza" kaiiba maiti kisirisiri kaenda nayo. Wengi kama hao wamepita duniani ambao kaumu yao au wafuasi wao walikuwa na itikadi hii hii kuwa maiti yake ilipotea ikaingia peponi pamoja na mwili wake. Sasa, je Wakristo watakubali kwamba kweli huenda ilitokea hivi hivi. Kwa mfano, msiende mbali, yaangalieni matukio ya bwana Baba Nanak. Wafuasi wake

Masingasinga laki kumi na saba wanaafiki kuwa kwa hakika baada ya kufariki yeye aliingia peponi pamoja na mwili wake, na sio kuafikiana tu bali ndivyo ilivyoandikwa katika vitabu vyao vyenye kuaminika vilivyoandikwa katika zama hizo hizo. Sasa je Wakristo wanaweza kukubali kuwa kwa kweli Baba Nanak amekwenda peponi na mwili wake? Ni masikitiko kuwa Wakristo wanakumbuka falsafa kwa wengine, lakini kwa mambo yao yasio ya akili wanaiweka falsafa kando kabisa! Kama Wakristo wakitaka kufanya uadilifu kidogo wanaweza kuelewa haraka kwamba hoja ya Masingasigna juu ya kupotea kwa mwili wa Baba Nanak na kwenda peponi pamoja na mwili wake ni madhubuti na zastahili kufikiriwa kuliko mapiswa ya Wakristo na bila shaka ni zenye nguvu kuliko hoja za Injili. Kwani, kwanza matukio hayo yaliandikwa ndani ya Janamsakhi ya Bala wakati uo huo, lakini Injili ziliandikwa miaka mingi baada ya zama za Yesu. Kisha jambo lingine litialo uzito tukio la Baba Nanak ni kuwa yaonekana karama inayonasibishwa kwa Yesu, kwa kweli, ndiyo kwa kuficha aibu waliyoipata wanafunzi wa Yesu mbele ya Mayahudi. Kwani pale Mayahudi walipomtundika Yesu msalabani, kisha wakamuomba mwujiza huu kwamba yeye akifufuka ashuke sasa hivi kutoka msalabani, basi tutamwamini, lakini wakati huo Yesu hakuweza kushuka kutoka msalabani. Kwa sababu

hiyo wanafunzi wa Yesu wakaaibika sana, wakashindwa kukabiliana na Wayahudi. Hivyo, kwa kuficha aibu yao ilikuwa hakuna budi wafanye hila fulani ambayo kwayo waepukane na shutuma, kejeli na dhihaka machoni mwa wenye akili chache. Hivyo, akili inalikubali jambo hili kuwa kwa kufutilia mbali doa la fedheha usoni mwao, lazima watakuwa wamefanya hila hii kuwa wakati wa usiku kama walivyotuhumiwa kufanya, maiti ya Yesu wakaitoa kaburini na kuiweka ndani ya kaburi lingine. Kisha sawa na msemo maarufu wa (*Kipanjabi*), 'Shahidi wa Bwana Khwaja ni chura' — yaani hakuna shahidi isipokuwa mdai mwenyewe ndiye shahidi wake — wakasema kuwa angalieni Yesu, mlivyokuwa mnamwomba, amefufuka, lakini amepaa mbinguni! Lakini matatizo hayo hayakuwapata Masingasinga alipokufa Baba Nanak wala hakuna adui aliyewashutumu kwa hiyo, wala haikutokea haja ya kufanya ujanja kama huo wala yeyote hakupiga kelele kama walivyopiga kelele Mayahudi kuwa maiti imeibiwa. Basi, kama Wakristo wangekuwa na itikadi hiyo kumhusu Baba Nanak badala ya Yesu, ingeingia akilini kidogo, lakini fikara hiyo kumhusu Yesu imejaa uvundo wa uzushi dhahiri na udhanganyifu.

Udhuru wa mwisho unaotolewa juu ya kuteswa kwa Yesu na kufishwa msalabani ni huu kuwa yeye akiwa

Mungu akatundikwa msalabani ili kifo chake kiwe kafara kwa wenye dhambi. Lakini jambo hili nalo limebuniwa tu na Wakristo kuwa Mungu pia huwa anakufa, ingawa baada ya kufa wakamfufua na kumfikisha kwenye arshi. Na bado wamenaswa ndani ya dhana hii batili kuwa atakuja tena duniani kuhukumu na mwili alioupata mara ya pili baada ya kufa, mwili ule ule akiwa mungu utakuwa naye daima dawamu. Sasa huyo mungu mwenye mwili wa Wakristo sawa na kauli yao ameshafikiwa na mauti pia safari moja, na ana damu, nyama, mifupa na viungo vyote vya juu na chini, huyo anafanana na *ma-Autar* wa Mabaniani ambao siku hizi Waaria wanaendelea kuwaacha kwa jazba sana. Tofauti yenyewe ni hii tu kuwa mungu wa Wakristo alizaliwa mara moja tu kutoka katika tumbo la Mariamu binti Yakubu, lakini mungu wa Mabaniani, Bishnu, akakubali mara tisa kutiwa doa hilo la kuzaliwa kwa ajili ya kuiondolea dunia dhambi. Hususan kisa cha kuzaliwa kwake kwa mara ya nane kinaelezwa kwa njia ya kuvutia sana. Wanasema kuwa ardhi ilipozidiwa na nguvu ya dhambi, Bishnu akapata kuzalika usiku wa manane kutoka katika tumbo la msichana na akadhihirika kimwili na akawaondolea watu dhambi zilizokuwa zimeenea duniani. Kisa hiki,

ingawa, kinaendana sawa na upendo wa Wakristo, lakini katika jambo hili Mabaniani walitumia akili sana kwamba wao hawakuwawamba *ma-Autar* wao msalabani kama Wakristo, wala hawaamini kuwa wao wamelaaniwa. Kutokana na baadhi ya ishara za Kurani Tukufu yafahamika waziwazi kuwa wazushi wa kwanza wa kumfanya mtu kuwa mungu ni ma-Barahman wa India kisha mawazo hayo Wayunani wakayachukua kutoka kwa Mabaniani, mwishoni katika itikadi hii makuruhu Wakristo wakawa wala kinyesi cha mataifa hayo mawili. Na Mabaniani wakawaza jambo moja la mbali ambalo Wakristo hawakuliwaza, nalo ni kwamba kwa Mabaniani ni kanuni ya kale ya Mungu Aliye tangu azali na wa milele kuwa kila dunia ilipojaa dhambi, Parmeshar wao akafikiria mbinu hii tu kuwa yeye mwenyewe apate kuzaliwa duniani akawaokoe watu. Na tukio hili halikutukia mara moja tu bali likatukia sikuzote katika nyakati za dharura. Lakini, ingawa Wakristo wanayo itikadi hii kuwa Mwenyezi Mungu ni tangu azali, na tukiendelea kurudi nyuma sana hata kiasi gani kwa zama zilizopita, mwanzo wa uwepo wa Mungu huyo haupo, na tangu azali Yu Muumbaji na Mola wa walimwengu pia. Lakini hawakubali kuwa yeye daima, tangu zama zisizo na kikomo alikuwa

ameendelea kuwatundika wanawe wapendwa msalabani kwa ajili ya watu. Bali, wanasema kuwa utaratibu huu kaufikiria hivi karibuni, na sasa hivi baba mkongwe amepata wazo hili kuwa amfishe mwanaye msalabani akawaokoe wengine katika adhabu. Hii ni dhahiri kwamba kwa kulikubali jambo hili kuwa Mungu ni wa kale na Ameendelea tangu azali, yalazimu kukubali jambo hili la pili pia kuwa viumbe vyake navyo kispishi vimeendelea kuwepo tangu azali. Na kwa sababu ya madhihirisho ya tangu kale ya sifa za tangu kale, ulimwengu mmoja ulioweza kuwepo pengine uliendelea kufichika kwa kutoweka na badala yake pengine ulimwengu mwingine uliendelea kudhihirika. Na hakuna yeyote awezaye kuhesabu kuwa ma-ulimwengu mangapi Mungu Aliyaondoa kutoka dunia hii na badala yake akayaleta ma-ulimwengu mengine. Mwenyezi Mungu Akisema ndani ya Kurani Tukufu kuwa Sisi Tuliumba majinni kabla ya Adamu ameashiria kwenye uwepo uo huo wa kale wa spishi ya ulimwengu. Lakini juu ya ithibati dhahiri ya ulazima wa uwepo wa kale wa spishi ya ulimwengu mpaka sasa hawajaleta orodha yoyote ya kujulisha katika ma-ulimwengu hayo yasiyohesabika yaliyotengana kila mmoja na mwingine, ni mara ngapi mwana wa mungu aliwambwa msalabani. Kwani ni

dhahiri kuwa sawa na fundisho la dini ya Kikristo hakuna mtu asiyekuwa na dhambi isipokuwa mwana wa Mungu. Hivyo, katika hali hii hakuna budi kuuliza kuwa viumbe waliopita hata kabla ya Adamu wetu huyu ambao hawakuwa na uhusiano wowote na silsila ya wanadamu hawa, ulifanyika mpango gani kwa msamaha wa dhambi zao? Na je ni mtoto huyu huyu ambaye mara nyingi hapo kabla aliwambwa msalabani kwa ajili ya kuwaokoa au alikuwa ni mtoto mwingine aliyekuwa akiwambwa msalabani kwa ajili ya viumbe wa zama zilizopita? Kadri tufikirivyo, tunaelewa kuwa kama hakuna msamaha wa dhambi bila msalaba, basi mungu wa Wakristo atakuwa na watoto wengi wasiohesabika ambao katika nyakati mbalimbali watakuwa wameuliwa katika nyanja hizo, na kila mmoja katika wakati wake atakuwa amewambwa msalabani. Hivyo, ni bure kabisa kutarajia manufaa yoyote kutoka kwa mungu kama huyu aliyeendelea kufiwa na vijana wake mwenyewe.

Katika mjadala wa Amritsar pia tuliuliza swali hili kwamba Wakristo wanakubali kuwa Mungu wao hataki kumwangamiza yeyote katika dhambi, sasa katika hali hii wanaulizwa kuwa Mungu huyo aliandaa mpango gani kwa kuziokoa roho chafu za mashetani, roho chafu ambazo zimetajwa ndani ya

Injili.[1] Je amewahi kuja duniani mwana yeyote aliyetoa uhai wake kwa ajili ya dhambi za mashetani, au aliwazuia mashetani kutenda dhambi. Kama mpango wa aina hii haukufanyika, basi inathibitika kuwa Mungu wa Wakristo daima aliridhika awateketeze katika jahanamu ya kudumu mashetani ambao kwa kauli za Wakristo ni wengi kuliko hata wanadamu. Tena, kwa vile habari yoyote ya mwana kama huyo haikutolewa, hapo iliwabidi Wakristo kukiri kuwa Mungu wao aliwaumba mashetani kwa ajili ya

[1] Tanbihi: Kutokana na mafundisho ya Kiislamu, inathibitika kuwa mashetani pia huwa wanaamini. Seyidna na Maulana Mtume s.a.w. alisema kuwa shetani wangu amekwishasilimu. Ilmuradi, kila mtu ana shetani wake, na shetani wa mtu mtawa aliyemkurubia Mungu huwa anaamini. Lakini inasikitisha kuwa shetani wa Yesu hakuweza kuamini, bali kinyume chake akamfikiria njia ya kumpoteza, akampeleka kwenye mlima mmoja na kumuonyesha mali za dunia na akamwahidi kuwa akimsujudia atampa mali hizo zote. Kauli hiyo ya shetani kwa hakika ilikuwa na bishara kubwa, na iliashiria pia kuwa taifa la Kikristo litakapomsujudia litapatiwa mali zote ya duniani, na ndivyo ilivyotokea. Wale ambao kiongozi wao baada ya kuitwa Mungu akamfuata shetani, yaani akamfuata nyuma yake, haikuwa muhali kwao kumsujudia shetani. Ilmuradi, mali zote za Wakristo kwa kweli zinatokana na sijida hii hii yao kwa shetani. Na ni dhahiri kuwa sawa na ahadi ya kishetani Wakristo walipewa mali za dunia baada ya sijida hiyo. Mwandishi.

jahanamu tu. Ilmuradi, maskini Wakristo tangu walipomfanya mwana wa Mariamu kuwa Mungu, wamo ndani ya misiba mikubwa mikubwa. Hakutakuwa na siku ambapo roho zao wenyewe hazitakuwa zinaichukia itikadi hiyo. Kisha msiba mwingine waliokabili ni kuwa baada ya utafiti lengo lolote la aliyesulubiwa halithibitiki katu, wala haithibitiki faida yoyote ya kutundikwa kwake msalabani. Kwani hapa pana sura mbili tu:

(1) Mosi, wamwekee mwana huyu marehemu shabaha ya kusulubiwa kuwa awajasirishe wafuasi wake kutenda dhambi, na kwa kutegemea kafara yake aeneze ufasiki, na kila aina ya upujufu kwa nguvu sana. Lakini, shabaha hii ndio upuuzi dhahiri na ni njia ya kishetani. Nadhani duniani hatakuwepo mtu atakayeipendelea njia hii ya kifasiki na kumchukua mwanzilishi wa dini kama hiyo kuwa mwema aliyewahimiza watu kwa jumla kufanya dhambi. Bali kwa tajiriba imejulikana kuwa fatwa kama hii hutoa wale tu ambao kwa kweli hukosa imani na mwenendo mwema na kwa sababu ya tamaa zao za nafsi walitaka kuwatumbukiza wengine pia katika jahanamu ya maovu. Na kwa kweli watu hao wanashabihiana na wale wanajimu wanaojikalia barabarani na kuwadanganya wapita njia, na kwa kuchukua pesa moja moja wanawatolea wajinga hao bishara kwa maneno ya kuwatuliza kuwa ni karibu bahati yao

njema ifunguke. Na kwa kujifanya sura yao kama ya mchunguzi wa kweli huangalia kwa makini sana mistari kwenye kiganja chao na umbo la uso wao kama kwamba wanataka kugundua baadhi ya alama fulani, kisha kwa kupekua pekua kurasa za kitabu fulani cha kuonyesha tu kilichowekwa mbele yao kwa shabaha hiyo ya kudanganya huhakikisha kuwa nyota kubwa ya bahati ya huyo mteja iko karibu kung'aa, huenda huyo atakuwa mfalme wa nchi fulani, waila uwaziri uwepo tu. Au, watu hao ambao juu ya machafu ya kudumu ya mtu fulani wanataka kumfanya kuwa mwenye kuteremkiwa fadhili ya Allah, ni kama waalkemia ambao kwa kumwona mwenye akili kidogo, lakini tajiri, wanataka kumwinda kwa maneno ya kujinata. Na kwa kusema maneno mbalimblai yasiyohusikana wanaanza kuwalaumu waalkemia wa awali kwamba hao waongo, waovu hunyakua mali za watu kwa udanganyifu bila haki kama wezi. Na hatimaye baada ya kurefusha maneno wanaishia kusema kwamba enyi mabwana, mdai yeyote wa alkemia niliyemuona katika umri wangu wa miaka hamsini, sitini, nimemkuta mwongo tu. Naam, mwalimu wangu marehemu alikuwa mualkemia wa kweli. Alitoa sadaka ya mamilioni ya rupia, nami kwa bahati nzuri nilipata heshima ya kumtumikia miaka kumi na miwili na nikapata matunda yake. Kwa kusikia

'kupata matunda', mjinga mmoja husema, mzee, bila shaka ukajifunza elimu ya alkemia kutoka kwa mwalimu wako. Akisikia hayo, mzee hukasirika kidogo na akikunja kipaji husema, bwana wee, usiliseme hilo, maelfu ya watu watakusanyika hapa, nasi twawakimbia kwa kujificha. Ilmuradi, kwa maneno hayo tu machache, majahili hutegeka, kisha haibaki shida yoyote ya kumchinja aliyekwisha tegwa tayari. Huwa wanamfahamisha kisiri faraghani kwamba bahati yako tu njema, kwa hakika, imetuvuta kuleta hapa kutoka maelfu ya maili, hata nasi tunashangaa kuwa moyo huu mgumu umelainikaje kwa ajili yako. Sasa fanya haraka ukalete kutoka nyumbani au hata kwa kumwomba mwingine dhahabu yenye thamani ya rupia elfu kumi, katika usiku mmoja tu itaongezeka kuwa mara kumi. Lakini, angalia, usimpashe habari yangu mtu yeyote, uombe kwa udhuru mwingine. Kwa kifupi, hatimaye wakijipatia dhahabu wanakwenda zao, na wale wajinga wenye tamaa ya kupata mara kumi hubakia kujililia tu. Hii ndiyo taabu ya uchu ule ambao kwa kughafilika na kanuni ya asili unafikishwa hadi mwisho. Lakini nimepata kusikia kuwa wadanganyifu kama hao hulazimika kusema kuwa waliokuja kabla yetu au watakaokuja baadaye, eleweni kwa yakini kuwa wote hao ni wadanganyifu, majambazi, wachafu, waongo hawanayo habari ya mbinu hii.

Vivyo hivyo Wakristo pia hawawezi kuimarika pasipo kuwafanyia manabii wote watukufu, kuanzia Hadhrat Adamu mpaka mwisho, kuwa wenye dhambi na waovu.[2]

(2) Sura ya pili ya kutundikwa msalabani kwa mtoto huyu anayestahili huruma ni hii kuwa wanaomwamini wataepukana na kila aina ya dhambi na maovu, na hazitapata kudhihirika jazba za nafsi zao. Lakini, ni masikitiko kuwa kama vile njia ya kwanza ilithibitika kuwa ni kinyume cha ustaarabu na kosa lake liko dhahiri, vivyo hivyo njia hii pia inathibitika waziwazi kuwa ni batili. Maana, ikidhaniwa kwamba katika kuamini kafara ya Yesu kuna sifa maalum kuwa mwenye imani ya kweli juu yake hugeuka kama malaika, na baada ya hapo wazo la dhambi haliingii moyoni mwake kabisa, basi tutalazimika kusema kuhusiana na Manabii wote waliopita kuwa hao hawakuamini kwa kweli msalaba wala kafara ya Yesu, kwani kutokana na kauli za Wakristo, hao walipita kiasi katika maovu. Miongoni

[2] Tanbihi: Akili na ufahamu wa Wakristo vinasikitisha kuwa hao kwa kumfanya Yesu kuwa Mungu hawakumnufaisha kitu, bali wakamfedhehesha tu mbele ya watu wema. Ingekuwa bora kwamba kwa kuifikishia roho yake thawabu wangetoa sadaka, wangemuombea dua ili mwisho wake ungekuwa mwema. Ilifaa nini kumfanya mtu kuwa Mungu. — Mwandishi.

mwao yumo aliyeabudu masanamu na yupo aliyeua bila haki, kuna aliyefanya maovu na binti zake mwenyewe, na hususan babu yake Yesu, Daudi alifanya matendo yote mabaya. Yeye kwa ujanja akamwulisha mtu asiye na dhambi kwa ukware wake, akatuma wanawake makuwadi wamlete mkewe, akamnywesha pombe na akazini naye, na akapoteza mali nyingi katika uzinzi. Na maisha yote akawa na wake kufikia mia moja, na kitendo hiki pia sawa na kauli ya Wakristo kilihesabiwa kuwa uzinzi. Na ajabu zaidi ni kwamba roho mtakatifu alikuwa anamshukia yeye kila siku, na Zaburi ilikuwa inashuka kwa bidii. Lakini, ni masikitiko kuwa si roho mtakatifu wala imani juu ya kafara ya Yesu iliyomzuia kutenda maovu, na mwishowe akafa ndani ya maovu hayo. Na ajabu kubwa zaidi ni kwamba kafara hiyo haikuweza kuwazuia bibi zake Yesu (kwa baba na mama) wasitende maovu, ilhali kwa maovu hayo asili ya Yesu ilitiliwa doa. Na bibi zake hao si mmoja au wawili bali ni watatu. Bibi mmoja mkubwa wa Yesu (kwa mama), na kwa nija nyingine alikuwa kwa baba pia, yaani Rahabu, alikuwa malaya, yaani kahaba. Tazameni (Yeshua 2:1). Na bibi yake mwingine (kwa mama), na kwa nija nyingine alikuwa kwa baba pia, jina lake Tamar, huyu alikuwa muovu kama makahaba wasio na leseni. Tazameni: Mwanzo (38:16-30) Na bibi mwingine tena wa Bwana Yesu (kwa mama), na kwa

njia nyingine alikuwa kwa baba pia, anaitwa Bath-sheba, huyu ndiye yule 'mwema' aliyefanya kitendo cha zinaa na Daud[3]. Tazameni: 2 Samueli 11:3

Sasa ni dhahiri kuwa lazima hao bibi zake Yesu kwa baba na mama walikuwa wamearifiwa juu ya kafara ya Yesu, nao watakuwa wameiamini. Kwani, ni fundisho la Wakristo kuwa manabii waliopita na nyimati zao pia walipewa mafundisho haya haya ya kafara na wakaokoka kwa kuiamini. Basi, kama athari ya Yesu kusulubiwa ikifahamika kuwa mtu kwa kuamini juu ya kusulubiwa kwake huepukana na dhambi, ilitakiwa kuwa bibi zake Yesu wa ubabani na umamani wangelindwa na uzinzi na uasherati. Lakini kwa kuwa mitume wote — ingawa kulingana na kauli ya Wakristo, waliamini kujiua kwa Yesu — hawakuweza kusalimika na maovu, wala bibi zake wa ubabani na umamani hawakuweza kusalimika, basi imethibitika kwa uwazi kuwa kafara hii ya uongo haiwezi kumsalimisha yeyote kwa tamaa za nafsi wala

---

[3] Seyidna na Maulana Mtume[saw] anasema kwamba kuanzia mama yangu hadi Bi Hawa, katika mfululizo wa mama zangu hakuna mwanawake yeyote aliye mwasherati wala mzinifu, wala hakuna mwanamume mzinzi na mwasherati. Lakini kulingana na kauli ya Wakristo katika uzazi wa Bwana mungu wao kuna damu ya wanawake watatu wazinifu, ilhali iliyoandikwa katika Torati kukihusu kizazi cha wanawake wazinifu, haikufichika kwa yeyote. — Mwandishi.

haikuweza kumsalimisha hata Yesu mwenyewe. Hebu angalieni alivyomfuata-fuata shetani nyuma yake[4],

---

[4] Wanafalsafa wa kizungu wa siku hizi, ingawa ni Wakristo, hawaamini kuwa kweli shetani akimrubuni Yesu akampeleka kwenye mlima mmoja, kwani hao hawaamini kuwa shetani ana mwili, bali wanakana kuwepo kwa shetani. Lakini kwa kweli mbali na mawazo ya wanafalsafa hao kuna kipingamizi hapa kuwa kama tukio hili la usuhuba na shetani lingefanyika kwenye milima ya Mayahudi na njia zao, siyo Yesu peke yake bali lazima Mayahudi wengi pia wangemuona shetani huyo. Na hakuna shaka kuwa shetani hatakuwa kama mwanadamu wa kawaida, bali atakuwa ni kiumbe wa sura ya ajabu mwenye kuwastaajabisha wamtazamao. Hivyo, kama Yesu alimuona shetani akiwa macho siyo usingizini, basi kwa kumuona maelfu ya Mayahudi na watu wengine walitakiwa kukusanyika hapo, na kungekuwa na kusanyiko kubwa, lakini haikutokea hivyo. Basi, watafiti wa Kizungu hawawezi kukubali kuwa tuko hili lililotokea kidhahiri, bali kwa sababu ya mawazo mabovu kama hayo ambamo lipo dai la uungu pia, wanajitenga na Injili. Hivyo, hivi karibuni mtaalamu mmoja wa kizungu alieleza maoni yake kuhusiana na Injili takatifu ya Wakristo kuwa katika rai yangu kwa kumhakikishia mtu mwenye busara kuwa Injili ni tungo la watu bali ni uvumbuzi wa kishenzi mtu huyo anahitaji tu aisome Injili. Kisha Bwana huyo anasema, mwisome Injili kama mnavyosoma kitabu kingine chochote kiwacho, na muifikirie kama mnavyovifikiria vitabu vingine, muifutilie mbali machoni mwenu ile staha yake na mjiondolee kicho chake moyoni mwenu na mtoweshe wasiwasi ubongoni mwenu, kisha muisome Injili takatifu, ndipo mtashangaa kuwa kwa nini mlimdhania mwandishi huyo wa ujahili na udhalimu hata kwa muda mfupi tu kuwa mwenye akili, mwema na mtakatifu.

ilhali haikumpasa kwenda. Na pengine hicho ndicho kitendo kilichomfanya ajute sana kiasi hiki kwamba mtu mmoja alipomwita mwema, yeye akamzuia

---

Kadhalika wapo wanafalsafa na wanasayansi wengi ambao wanaitazama Injili kwa chuki sana, na kwa sababu ya mafundisho yake yasiyotakasika wameichukia*, ambayo kwa mtu mwenye akili kuyaamini kwa hakika ni fedheha. Kwa mfano, kisa hiki cha uongo kwamba kuna baba mmoja mwenye hasira kali, anataka kuwaua wote, na kuna mwana mwenye huruma sana ambaye akawaepusha watu na hasira ya kimajnuni ya baba yake kwa kujisulubisha. Sasa maskini watafiti wa Ulaya wayaaminije mambo kama hayo ya upuuzi. Vivyo hivyo yalivyo mawazo ya kijahili ya Wakristo, wakamgawanya Mungu katika miili mitatu: mwili mmoja ambao utabakia milele kwa sura ya mtu, jina lake mwana wa Mungu, mwili wa pili utakaobakia daima kwa sura ya njiwa, jina lake Roho Mtakatifu, na mwili wa tatu ambao Mwana kajikalia kuumeni kwake. Sasa mtu mwenye akili aaminije miili mitatu! Lakini tuhuma ya kufuatana na shetani siyo chekesho kidogo kwa wanafalsafa wa Ulaya. Baada ya juhudi kubwa maelezo yanatolewa

---

*Tanbihi: Miongoni mwa Wakristo, mtu yeyote kadiri anavyofikia kilele cha falsafa, ndivyo hivyo anavyochukia Injili na dini ya Kikristo, hata kwamba katika siku hizi kuna mama mmoja wa kizungu ambaye ametoa kijitabu kimoja cha kubatilisha imani ya Kikristo, lakini hali ya wanafalsafa wa Kiislamu ni kinyume na hiyo. Bu Ali Sina ambaye anajulikana kuwa mkuu wa wanafalsafa na mwenye imani mbovu na mwasi wa dini, yeye anaandika mwishoni mwa kitabu chake 'Isharati' kwamba ingawa dalili za kifalsafa hazipo juu ya ufufuo wa miili bali zipo kwa kinyume chake, lakini kwa kuwa Mtoa habari Mkweli s.a.w. ameshasema kwa hiyo tunauamini. —Mwandishi

akisema kwa nini unaniita mwema! Kwa kweli mtu aliyemfuata shetani atawezaje kujasiri kusema mimi ni

---

kuwa hali hizo zilitokana na mawazo ya nguvu za akili ya Yesu mwenyewe. Na wanalikubali pia kuwa katika hali ya afya njema mawazo hayo yachukizayo hayawezi kuzalika. Ni uchunguzi wa watu wengi kuwa ndivyo wenye kifafa mara nyingi wanavyowaona mashetani, na ndivyo wanavyoeleza kuwa shetani alitupeleka sehemu fulani fulani, katuonyesha maajabu kadha wa kadha. Nami nakumbuka kuwa labda miaka thelathini na minne hivi imepita niliona ndani ya ndoto kwamba sehemu fulani shetani mweusi mwenye sura mbaya amesimama, kwanza alinielekea mimi, nami nikimpiga kofi usoni nikasema ondoka ewe shetani, wewe huna sehemu ndani yangu. Kisha akamuelekea mwingine na kumchukua pamoja naye, na yule aliyemchukua naye nilikuwa namjua, kisha nikaamka. Siku hiyo hiyo au baada yake mtu yule akashambuliwa na kifafa, niliyemuona ndani ya ndoto kwamba alichukuliwa na shetani, naye akakumbwa na ugonjwa wa kifafa. Hapo nikapata yakini kuwa uaguzi wa kuwa na shetani ni kifafa. Hivyo basi, hii ni nukta ya kina na ni rai safi na yenye akili kwamba kwa kweli Yesu alikuwa anaugua ugonjwa wa kifafa, na ndiyo maana alikuwa akiota ndoto za namna hiyo, na shutuma ya Mayahudi kuwa unafanya mambo kama hayo kwa msaada wa Beelzebuli inaunga mkono rai hii na inatuliza, kwani Beelzebuli pia ni jina la shetani. Na kauli ya Mayahudi kwa sababu hii pia yaweza kuwa sahihi na kuaminika kwa kuwa wale watu wanaopagawa na shetani na shetani huanza kuwapenda, na ingawa kifafa chao wenyewe hakiponi, lakini huweza kuwaponya wengine, maana shetani huwapenda na hapendi kutengana nao, na kwa sababu ya upendo wao mwingi hukubali maneno yao na kwa ajili yao huwaponyeshea wengine maradhi yao ya kishetani. Na watu wa hali hii daima hutumia ulevi

mwema! Ni jambo la hakika kabisa kuwa Yesu kwa

---

na vitu vichafu, nao huwa ni walevi na walafi wa hali ya juu. Muda kidogo umepita, mtu mmoja alikuwa kakumbwa na maradhi ya aina hiyo ya kuzimia, yasemekana kuwa yeye alikuwa akitoa majini ya wengine. Ilmuradi, tukio hili la Yesu kuwa pamoja na shetani ni dalili iliyo wazi ya ugonjwa wake wa kifafa. Nasi tuna dalili nyingi ambazo hakuna haja ya kuziandika kwa kirefu hivi sasa, na tuna yakini kuwa watafiti wa Kikristo ambao mapema wanaafikiana na rai yetu hii hawatakataa. Na mapadri majahili wakikataa, basi wanatakiwa watoe uthibitisho kuwa Yesu kule kufuatana na shetani kwa kweli ni tukio lililotokea katika hali ya kuwa macho siyo usingizini* wala haikutokana na maradhi ya kifafa. Lakini, kwa kuthibitisha hiyo waletwe mashahidi wa kuaminika waliojionea wenyewe. Na inaonekana kuwa kushuka kwa njiwa na kutamka u mwanangu mpendwa, kwa kweli pia ni kukumbwa na kifafa ambacho kwacho yakazalika mawazo kama hayo. Ni hivi kuwa rangi ya njiwa huwa nyeupe, na rangi ya balaghamu pia ni nyeupe na maada ya kifafa ndiyo balaghamu tu. Basi balaghamu ilionekana kwa sura ya njiwa. Na kule kusema kuwa u mwanangu, ndani yake mna siri hii kuwa mwenye kifafa huwa mtoto wa kifafa, ndiyo maana ndani ya fani ya utabibu kifafa huitwa Ummus-Sibyani, yaani mama wa watoto. Na safari moja nduguze wote wanne wa Yesu waliipelekea Serikali ya wakati ule ombi pia kuwa mtu huyu (Yesu) amepatwa na kichaa, afadhali ashughulikiwe yaani atiwe katika jela ya mahakamani ili atibiwe kufuatana na desturi za huko. Basi, ombi hili pia ni dalili dhahiri kwa jambo hili kuwa kwa kweli kutokana na maradhi ya kifafa Yesu alikuwa amepata kichaa. Mwandishi.

---

*Swali ni hili kuwa kina nani waliomuona Yesu pamoja na shetani.

fikara yake na kutokana na baadhi ya mambo mengine pia akajitenga na kuitwa mwema. Lakini ni masikitiko kuwa sasa Wakristo si tu wanamchukua kuwa mwema, bali wakamfanya Mungu. Ilmuradi, kafara haikumfaa kitu Yesu mwenyewe pia, na kiburi na majivuno ambayo ndiyo mzizi wa maovu yote, yaonekana imekuwa ndiyo sehemu ya Bwana Yesu. Kwani, kwa kujifanya Mungu amewaita manabii wote kuwa majambazi na wezi na watu wachafu, ilhali ikirari hii inatokana na kauli yake kuwa yeye mwenyewe si mwema. Lakini ni masikitiko kuwa mafuriko ya kiburi yameiangamiza kabisa hali yake yote. Mtu mwema hawalaumu watawa waliopita, lakini yeye amewaita manabii watakatifu kuwa majambazi na wanyang'anyi. Daima amezoea kuwaita wengine kuwa 'wadanganyifu' na 'waovu', hakutumia neno la adabu kwa mtu yeyote, kwani si mwana wa Mungu huyo!! Na tunapoangalia kuwa kafara ya Yesu imewatilia wanafunzi wake athari gani nyoyoni mwao, je, kwa kuiamini hiyo wakaepukana na dhambi, hapo pia hamna utakaso wa kweli. Hii ni dhahiri kuwa watu hao walikwishaamini baada ya kusikia tukio la kutundikwa msalabani, hata hivyo matokeo yakawa kwamba wakati wa Yesu kukamatwa, Petro akisimama mbele yake akamlaani, wengine wote nao wakamkimbia, na nuru ya itikadi haikubakia ndani ya moyo wa yeyote. Kisha baada ya

hapo, hali ya kuepukana na dhambi mpaka sasa ni hii kuwa hasa kwa ikirari za watafiti wa Ulaya inathibitika kuwa uasherati umezidi katika Ulaya kiasi hiki kwamba mjini London maelfu ya wanaharam wanazaliwa kila mwaka. Na mambo machafu sana ya Ulaya yamechapishwa yasiyostahili kusemwa na kusikia. Unywaji wa pombe umekithiri kiasi hiki kuwa kama maduka ya pombe yapangwe katika msitari, pengine yasiishie hata kama msafiri akiisha safiri vituo viwili. Hakuna ibada, usiku na mchana hakuna shughuli nyingine isipokuwa anasa na kushughulikia mambo ya dunia tu. Hivyo basi, utafiti wote huo unathibitisha kuwa kwa Yesu kusulubiwa walioamini hawakuweza kuacha dhambi,[5] bali kama vile mkondo mkali wa maji ya mto unvyoangamiza vijiji vya pembeni pindi ukuta wa kuzuia maji uliojengwa ukingoni mwa mto ubomokapo, ndivyo ilivyo hali ya wanaoamini kafara. Nami najua kuwa Wakristo hawataijadili sana, maana ikiwa manabii waliojiwa na malaika wa Mungu,

[5] Tanbihi: Kusulubiwa kwa Yesu kama kungetokana na ridhaa yake mwenyewe, kungekuwa ni kujiua na kifo cha haramu; na katika hali ya kutokuridhia kifo hakiwezi kuwa kafara. Na Yesu mwenyewe hakuweza kujiandika mwema, kwani watu walijua kuwa mtu huyu ni mlevi. Na mienendo hiyo mibaya siyo baada ya uungu, bali inaonekana ni tangu mwanzo tu. Hivyo basi, kujidai uungu ni tokeo moja la unywaji ulevi. — Mwandishi

kafara ya Yesu haikuweza kuwazuia na maovu, yawezaje kuwazuia wafanyabiashara na mafundi na mapadri wenye mawazo finyu kutenda matendo machafu. Ilmuradi, hali ya mungu wa Wakristo ndiyo tuliyoishaeleza.

Dini ya tatu mbali na dini hizo mbili tulizoziongelea sasa hivi ni Isalm. Utambuzi wa kiungu wa dini hii ni wazi sana na unawiana kabisa na asili ya mwanadamu. Kama vitabu vyote vya dini zote vitoweke na fikara zote na mawazo yao yote ya mafundisho yafutike, hata hivyo Yule Mungu Ambaye Kurani Tukufu inaelekeza kwake, Atadhihirika wazi wazi katika kanuni ya kudra, na sura yake iliyojaa uwezo na hekima itaonekana iking'aa ndani ya kila chembe. Ilmuradi, Mungu Yule ambaye Kurani Tukufu inatoa habari zake Hatawali viumbe wake kwa nguvu tu, bali kwa muafaka wa aya ya Kurani Tukufu:

أَلَسْتُ بِرَبِّكُمْ ۖ قَالُوا بَلَىٰ ۛ[6]

Kila chembe, kitabia na kiroho, inatii amri zake. Kwa kumwelekea Yeye, mvuto unapatikana katika kila tabia ya asili wala hakuna hata chembe isiyo na mvuto huu. Na hii ndiyo dalili moja kubwa juu ya kwamba Yu Muumbaji wa kila kitu, kwani nuru ya moyo inakubali kuwa mvuto ule wa kumwelekea Yeye

[6] Je Mimi si Mola wenu? Wakasema: Naam. Al-A'raaf, 7:173

unaopatikana ndani ya vitu vyote, bila shaka unatokana naye tu kama Kurani Tukufu ilivyoashiria hiyo katika aya hii:

وَإِنْ مِّنْ شَيْءٍ إِلَّا يُسَبِّحُ بِحَمْدِهِ[7]

Yaani, kila kitu kinamtukuza na kumsabihi. Kama Mungu hakuwa Muumba wa vitu hivi, kwa nini ndani ya vitu hivi mna mvuto wa kumuelekea Mungu? Mtu mwenye kutafakari lazima atalikubali jambo hili kuwa mvuto huu upo kwa sababu ya uhusiano uliofichika. Hivyo basi, kama uhusiano huu sio kwa sababu ya Mungu kuwa Muumbaji, basi Mwaria yeyote ajibu swali hili kuwa ndani ya Veda imeandikwa nini juu ya uhakika wa uhusiano huo, nao huo waitwa jina gani? Je, hii ndiyo kweli kuwa Mungu anatawala kila kitu kwa nguvu tu, na ndani ya vitu hivyo hakuna nguvu ya asili na shauku ya kuelekea kwa Mwenyezi Mungu? Mungu Apishe mbali, siyo hivyo, bali kudhania hivyo siyo upumbavu tu bali ni uhabithi wa hali ya juu. Lakini ni masikitiko kuwa Veda ya Waaria kwa kukataa uumbaji wa Mwenyezi Mungu haikuukubali uhusiano ule wa kiroho ambao ndiyo sababu ya utii wa kitabia wa kila kitu. Na kwa kuwa hao walikuwa mbali kabisa kabisa

[7] Banii Israaiil, 17:45

na maarifa ya kina na elimu ya keto, hivyo falsafa hii ya kweli ikafichikana kwao kwamba uhusiano wa asili wa miili yote na roho zote walazimu kwa Yule Dhati ambaye Yupo tangu azali. Na utawala wa Mungu sio wa bandia wala kwa nguvu tu, bali kila kitu kwa roho yake kinamsujudia Yeye, maana kila chembe imezama ndani ya ihsani zake zisizo na kikomo na imeumbwa naye. Lakini ni masikitiko kuwa wafuasi wa dini zote zenye upingamizi walijaribu kuzuia kwa nguvu mto mkubwa sana wa kudra na rehema na utukufu wa Mwenyezi Mungu kutokana na ufinyu wa moyo wao, na kwa sababu hizi miungu yao ya kubuni ikatiliwa madoa ya namna namna ya udhaifu, uchafu, uzushi, ghadhabu bila sababu na utawala usio halali. Lakini Islam haikuzuia popote pale mikondo yenye kasi ya sifa kamili za Mwenyezi Mungu, wala haifundishi kama Waaria kuamini kwamba roho za ardhini na mbinguni na chembechembe za miili ni miungu yao yenyewe, na yule aitwaye Parmeshar kutokana na sababu zisizojulikana anawatawala kama mfalme tu. Wala haifundishi kama dini ya Kikristo kuwa Mungu alizaliwa mithili ya mtu kutoka tumboni mwa mwanamke. Na si tu akameza damu ya hedhi kwa miezi tisa, na akajipatia damu, mifupu na nyama kupitia mwili wa mwenye dhambi, ambao mwili huo

katika tabia yake ulikuwa na sehemu ya uana kutoka kwa asili ya wanawake waovu kama Bath Sheba, na Tamari na Rahabu, bali akapata shida za magonjwa ya zama za utotoni kama vile taabu za surua, ndui, kuota meno n.k. akavumilia, na sehemu kubwa ya umri wake akapoteza kama watu wa kawaida na mwishowe alipokaribia kufa akakumbuka uungu. Lakini kwa vile lilikuwa ni dai tu tupu, na nguvu za uungu hakuwa nazo, hivyo alipodai tu akashikwa papo hapo. Lakini Uislamu unamwamini Mungu Mwenye jalali ya kweli kuwa Hanazo kabisa hali hizo zote pungufu na mbovu. Na pia inamwamini kuwa mbali kabisa na hasira kali mno kuwa asipate kukumbuka kuwasamehe waja wake mpaka awe amekwisha tia kitanzi shingoni mwa mtu fulani. Na kuhusu uwepo wa Mwenyezi Mungu na sifa zake, Kurani Tukufu inafundisha maarifa ya kweli matukufu na makamilifu kuwa kudra zake, rehema zake, adhma na utukufu wake hauna kikomo. Na ni dhambi yenye kuchukiza sana kwa mujibu wa mafundisho ya Kurani Tukufu kusema kwamba kudra na adhma, na rehema ya Mwenyezi Mungu huishia kwenye mpaka fulani, au baada ya kufikia sehemu fulani udhaifu wake unakuwa kikwazo kwake. Bali kudra zake zote huendelea sawa na kanuni hii imara kwamba kwa

kuacha mambo yaliyo kinyume cha utukufu wake, ukamilifu wake na sifa zake kamili, au ni kinyume cha ahadi zake zisizobadilika, mengine yote Anaweza kuyafanya Atakayo. Kwa mfano, hatuwezi kusema kwamba Anaweza kujifisha kwa kudra yake kamili, kwani hii ni kinyume cha sifa yake ya tangu azali ya kuwa Mwenye uzima na Mhifadhi wa milele. Sababu ni hii kuwa tangu awali Aliishadhihirisha kwa kitendo na kauli yake kuwa Yu tangu azali, ni wa kudumu, Hafi, wala haijuzu kwake kufa. Kadhalika hatuwezi kusema pia kuwa yeye anaingia ndani ya tumbo la mwanamke anameza damu ya hedhi, akikaa humo karibu miezi tisa, na kupata uzito wa ratili tatu, nne, anazaliwa kutoka katika utupu wa wanawake huku analialia. Kisha anakula chakula, anaenda haja kubwa na haja ndogo, na anaonja machungu yote ya dunia hii ya kupita, na mwishowe akipata mateso ya dakika chache ya gharighari ya mauti anaaga dunia hii isiyo ya kudumu, kwani mambo yote hayo ndiyo nakisi na upungufu na ni kinyume cha utukufu wake wa azali na ukamilifu utimilifu wake.

Kisha yapaswa kujua pia kwamba kwa vile katika itikadi za Kiislamu, Mwenyezi Mungu ndiye kwa hakika Muumba wa viumbe wote, zikiwemo roho na

maumbo, vyote vimeumbwa na Yeye na kutokana na nguvu zake vimepatikana. Hivyo basi, hii pia ni itikadi iliyofundishwa na Kurani Tukufu kwamba kama ambavyo Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuhuluku na kuumba kila kitu, vivyo hivyo Alivyo *Qayyum* pia, yaani kila kitu kinabaki kutokana na kuwepo kwake, na kuwepo kwake ndio kama uhai kwa kila kitu. Na kama Yeye Hayupo, basi hakuna kitu chochote. Ilmuradi, kwa kuwepo na kubaki kwa kila kitu, hakuna budi kuwepo Kwake. Lakini, hii siyo itikadi ya Waaria na Wakristo. Siyo ya Waaria kwa sababu hawamwamini Mwenyezi Mungu kuwa Muumbaji wa roho na maumbo, wala hawaamini uhusiano Wake na kila kitu unaothibitisha kuwa kila kitu ni natija ya kudra yake na nia yake tu, na ni kama kivuli kwa ajili ya matakwa yake. Bali wanachukulia kuwepo kwa kila kitu milele namna ambavyo yafahamika kuwa wanavidhania vitu vyote vipo kwa kudumu tangu azali na vipo vyenyewe. Basi, kwa kuwa vitu hivi vyote vilivyopo sawa na dhana yao vipo nje ya kudra ya Mwenyezi Mungu, kuwepo kwao siyo kwa sababu ya kudra yake, hivyo vitu hivi vyote pasipo shaka havina uhusiano na Parmeshar wa Mabaniani kiasi kwamba kama idhaniwe kuwa Parmeshar wao amekufa, hata hivyo roho na maumbo

havitapata tatizo lolote, maana Parmeshar wao ni kama mwashi tu. Na kama vile tofali na udongo havipo kwa sababu ya nguvu ya mwashi mwenyewe hata kwamba katika hali yoyote kuwepo kwao kumtegemee yeye, ndivyo ilivyo hali ya vitu vya Parmeshar wa Mabaniani. Basi, kama ambavyo kwa kufa kwa mwashi hailazimu kwa majengo yote aliyoyajenga maishani mwake yaporomoke papo hapo, ndivyo yasivyolazimu pia kuwa vitu vingine vipate shida kwa kufa kwa Parmeshar wa Mabaniani maana yeye si *Qayyuum*[8] wa hivyo vitu. Kama angekuwa *Qayyuum* lazima angekuwa pia muumbaji wao, kwani vile vitu visivyoihitaji nguvu ya Mungu katika kuumbika kwao, havihitaji pia msaada wa nguvu yake kwa kuendelea kubaki. Na sawa na itikadi ya Wakristo pia mungu wao mwenye mwili hawezi kuwa *Qayyuum* wa vitu, kwani ili kuwa *Qayyuum* lazima awe pamoja navyo. Na ni dhahiri kuwa mungu wa Wakristo, Yesu, hivi sasa hayupo ardhini, kwani kama angekuwepo ardhini, lazima angeonekana kwa watu kama alivyoonekana zama zile ambapo katika enzi ya Pilato alikuwapo nchini mwake. Hivyo, kwa kuwa hayupo ardhini iweje basi awe *Qayyuum* wa

[8] Kitu kischoumbika kwa kuitegemea kanuni asilia, hakiihitaji katu kanuni asilia kwa kubaki.

watu wa ardhini. Iliyobaki ni mbingu, yeye si *Qayyuum* wa mbingu pia. Kwani kiwiliwili chake kitakuwa karibu shibiri sita, saba tu, anawezaje kuwepo kotekote katika mbingu zote ili awe *Qayyuum* wao? Lakini sisi tunaomwita Mwenyezi Mungu kuwa Mola wa Arshi, hatumaanishi kuwa Yeye ana umbo na kiwiliwili na anahitaji Arshi. Bali, Arshi muradi wake ni pale pa juu palipotukuka panapohusiana kwa usawa na ulimwengu huu na ulimwengu ujao. Kule kusema kuwa Mwenyezi Mungu yuko juu ya Arsh kwamaanisha kwamba Yu Mmiliki wa dunia na akhera, na kama vile mtu akikaa pale palipo juu sana au akipanda juu ya jumba kubwa anavyoangalia kulia na kushoto, vivyo hivyo Mwenyezi Mungu alivyotambuliwa kiistiara kuwa Yuko juu ya kiti cha enzi kilicho juu sana na hakuna kitu kinachofichikana kwake – si cha dunia hii wala cha akhera. Naam, kwa wenye ufahamu wa kawaida hapo panaelezwa kwa upande wa juu, kwani maadamu Mwenyezi Mungu kwa kweli yuko juu kuliko vyote na kila kitu kimeangukia miguuni mwake, basi, Yeye Anahusiana na upande wa juu. Lakini upande wa juu ndiye Yule tu Ambaye dunia na akhera zipo chini yake. Na Yeye ni kama nukta ya juu kasisa ambapo kutoka chini yake yanatokea matawi

mawili ya ma-ulimwengu mawili makubwa, na kila tawi lina maelfu ya ma-ulimwengu ambayo hakuna anayeyajua isipokuwa Yule tu Ambaye Amestawi kwenye nukta hiyo ya juu kabisa inayoitwa jina Arshi (kiti cha enzi). Hivyo, kidhahiri pia ule upeo wa juu kabisa unaoweza kufikiriwa kwenye nukta hiyo ya mwisho iliyo juu ya ma-ulimwengu hayo mawili ndiyo huitwa Arshi katiak sheria. Na upeo huu wa juu kabisa kwa ujumla ndio wa Dhati Tukufu ya Mwumbaji ili iashiriwe kuwa Yeye ndiye chanzo cha kila upaji na ndiye Kimbilio la kila kitu, na ndiye Asujudiwaye na kila kiumbe na ndiye Aliye juu kuliko wote katika Dhati yake na sifa zake na ukamilifu wake, waila Kurani Tukufu inasema kuwa Yeye Yupo kila pahali kama ilivyosema:

اَيۡنَمَا تُوَلُّوۡا فَثَمَّ وَجۡهُ اللّٰهِ ؕ[9]

Popote mgeukiapo mtaukuta uso wa Mwenyezi Mungu. Inasema tena kuwa:

هُوَ مَعَكُمۡ اَيۡنَ مَا كُنۡتُمۡ ؕ[10]

Yu pamoja nanyi popote mlipo. Yasema tena:

وَنَحۡنُ اَقۡرَبُ اِلَيۡهِ مِنۡ حَبۡلِ الۡوَرِيۡدِ ○[11]

---

[9] Al-Baqara, 2:116

[10] Al-Hadiid, 57:5

Tu karibu naye zaidi kuliko halkumu yake. Hiyo ndiyo mifano ya mafundisho matatu.

Na amani iwe kwa yule aliyefuata muongozo.

---------------------------Mwisho---------------------------

Mpanga herufi za chapa
Mimi ndimi, Mnyenyekevu
Mpungufu wa elimu
Miongoni mwa wafuasi wa Masihi Mau'udi[as]
Ghulam Muhammad wa Amritsar

1 Desemba 1895, siku ya Jumapili.

[11] Qaaf, 50:17